Global Schools Program

MALENGO YA MAENDELEO ENDELEVU




# Muhtasari wa Kozi

## Darasa la 5

**Chanzo:** Reimers, F. (2017). *Empowering students to improve the world in sixty lessons*. 1st ed. Createspace Independent Publishing Platform.

**Hati Miliki:** © 2017 Fernando M. Reimers. Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya kimataifa ya Creative Commons Attribution 4.0. Kusoma nakala ya leseni hii tembelea, https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/ Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa:** Maudhui yote yaliyomo humu yameandaliwa na kuchapishwa na Programu ya Shule za Kimataifa (Global Schools Program).

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS
17 GOALS TO TRANSFORM OUR WORLD

Global Schools Program

| Muhtasari | |
|---|---|
| **Lengo la kujifunza**<br>Katika Darasa la 5, wanafunzi watajifunza kuhusu utofauti wa utamaduni, na mawasiliano kupitia lenzi ya dini. Kwa kujifunza kuhusu nafasi ya dini katika maisha yao wenyewe, jamii, na duniani kote, wanafunzi watafahamu utajiri wa tofauti za kiutamaduni. Wanafunzi pia, watajadili jinsi watu wanavyoweza kuwasiliana katika tofauti za kiutamaduni, na kuja pamoja kutatua matatizo. | |
| **Nguzo za Somo** | |
| **Somo la 1** | Maadili yangu yanahusianaje na maadili ya wengine? |
| **Somo la 2** | Dini ina mtazamo gani kwenye jamii yangu? |
| **Somo la 3** | Dini ulimwenguni kote |
| **Somo la 4** | Kuchunguza dini |
| **Somo la 5** | Mawasiliano, migogoro, na ushirikiano katika dini zote |
| **Madhumuni ya Kujifunza** | |
| • Wanafunzi watajifunza kuhusu tamaduni mpya, wakizingatia dini za ulimwengu.<br>• Wanafunzi watatafakari kwa kina kuhusu nafasi ya dini na taasisi nyingine za kiutamaduni katika jamii na maisha yao.<br>• Wanafunzi watatumia ujuzi wa mawasiliano na utatuzi wa changamoto ili kuendeleza njia za kutatua migogoro itakayoibuka. | |

**Darasa la 5 Somo la 1**

"Maadili yangu yanahusianaje na maadili ya wengine?"

**Muda:** Dakika: 60
**Mada:** Uraia, Historia, Maarifa ya Jamii
**Kiwango:** Elimu bora (SDG 4); Kupunguza kutokuwepo kwa usawa (SDG 10); Amani, Haki, na Taasisi thabiti (SDG 16).
**Imebuniwa na:** Isabelle Byusa, Arianna Pattek, Emily Papa, Sam (Shiv) Sharma, Tisha Verma, Devon Wilson

**Muhtasari na Mantiki:** Ili kuwawezesha wanafunzi kuchunguza muingiliano wa maadili na dini, wanafunzi watakamilisha zoezi ambapo wataeleza maadili yao wenyewe, na kisha kujadili jinsi dini mbalimbali zinavyoweza kulingana au kutolingana na maadili hayo. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi watapata ufahamu mkubwa zaidi wa kwa nini watu wanaamini na kuabudu kwa njia tofauti.

**Lengo la Ufundishaji:** Wanafunzi wataeleza maadili yao na kujifunza ni dini gani zinaweza kuendana au kutoendana na maadili yao.

**Lengo la Uelewa:** Kustawisha ustahimilivu kwa dini zote na kupata ufahamu wa kina na utambulisho wa mtu binafsi.

**Maswali muhimu ya kuzingatia:**

- Ustahimilivu wa kidini ni nini?
- Dini yako ni ipi na dini yako inathamini nini?
- Je, tunawezaje kujenga ustahimilivu na heshima kwa kuzingatia tofauti za kidini?

**Madhumuni ya wanafunzi kujifunza (Wanafunzi wataweza):**

- Kukuza ufahamu wa dini duniani/Ulimwenguni kote
- Kukuza uelewa wa mwingiliano kati ya dini na maadili yao
- Kukuza, kuthamini na kuheshimu tofauti za kidini

**Tathmini:** Wanafunzi wanaweza kuonesha uelewa wa maadili yao na jinsi yanavyohusiana na maadili ya darasa kwa ujumla.

**Mpangilio/Mtiririko wa Mazoezi**

- **Mwanzoni mwa Darasa**: Zungumza na wanafunzi kuhusu maadili, na uwaelekeze wanafunzi watafakari juu ya maadili yao na wabainishe maadili matano hadi kumi (5-10) ambayo ni muhimu zaidi kwao.

- **Anza:** Waambie wanafunzi watathmini jinsi maadili yao yanavyofanana na maadili ya wanafunzi wengine. Endesha majadiliano kuhusu jinsi maadili ya watu yanavyofanana au kutofautiana.

- **Baada ya hapo**, orodhesha maadili yaliyowekwa katika makundi, na uwaulize wanafunzi ni aina gani za maadili wanayojihusisha nayo zaidi na upige kura kwenye aina hiyo.

- **Kisha** wafafanulie wanafunzi maadili hayo yanaingiliana na dini gani.

  Kwenye mrengo wa kidini ➔ jadili na wanafunzi jinsi maadili na dini kutoka sehemu zote zinavyohusiana, na wapi zinatofautiana.

- **Jamii**: Jadili na wanafunzi namna dini ilivyo katika jamii.

- **Maswali ya kutafakari na kufanya utafiti wenyewe:**
  - Kuna dini ngapi duniani?
  - Tazama video ya Watu 100 (kiungo katika nyenzo hapa chini)
  - Chunguza kwa kina dini ya ukoo wa mtu

**Nyenzo kwa ajili ya wanafunzi:**
- Mradi wa Watu 100: https://www.100people.org/the-100-people-project-an-introduction/

**Nyenzo kwa ajili ya walimu:**
- Watu 100: https://www.100people.org/

**Darasa la 5 Somo la 2**

"Dini inatazamwaje katika jamii yangu?"

**Muda:** Dakika: 60
**Mada:** Uraia, Historia, Maarifa ya Jamii
**Viwango**: Elimu bora (SDG 4); Kupunguza kutokuwepo kwa usawa (SDG 10); Amani, Haki, na Taasisi thabiti (SDG 16)
**Imebuniwa na**: Isabelle Byusa, Arianna Pattek, Emily Papa, Sam (Shiv) Sharma, Tisha Verma, Devon Wilson

**Muhtasari na Mantiki:** Lengo la somo hili ni kuwasaidia wanafunzi kuwa na ufahamu na kutafakari juu ya nafasi zao katika ulimwengu huu wenye dini nyingi na kutafuta muingiliano wa dini hizi katika jumuiya zao na kwenye jamii zao.

**Lengo la Ufundishaji**: Wanafunzi watachunguza dini zilizopo katika jamii zao na kufikiria jinsi dini hizo zinavyotofautiana na zinavyoingiliana zenyewe kwa zenyewe na jamii kwa ujumla.

**Lengo la Uelewa**: Kujifunza kuhusu dini mbalimbali zilizopo katika jamii zao

**Maswali Muhimu:**
Je, tofauti katika dini inapaswa kuwa sababu ya jinsi tunavyowaona wanajamii wenzetu?

**Wanafunzi wataweza**: Kukuza ujuzi wa dini mbalimbali katika jumuiya za wanafunzi (au jamii kwa ujumla).

**Tathmini**: Wanafunzi wataweza kuonesha uelewa wa dini mbalimbali zilizopo katika jumuiya zao

**Mpangilio wa mazoezi:**

- Majadiliano ya darasa juu ya dini mbalimbali, kupitia upya maudhui kutoka somo la awali.
- Waelekeze wanafunzi wagawanyike katika vikundi na kuchunguza dini zinazopatikana katika jamii ya mtu, ama kwa kupitia vyanzo vya mtandaoni kama vile tovuti na video za YouTube au kwa kuwafanya wanafunzi watembee katika jumuiya yao ya karibu na kutembelea nyumba mbalimbali za ibada.
    - Aidha, wanafunzi wanaweza kutembelea na kuwa na taarifa za moja kwa moja kwenye tovuti tofauti za kidini.
- Majadiliano ya darasa ambayo wanafunzi watatafakari juu ya kile walichojifunza kuhusu dini mbalimbali katika jamii zao. Wanafunzi wanaweza kutaja jambo kubwa moja hadi

mawili (1 - 2) juu ya walichojifunza kutoka kwenye mada waliyojadiliana kwenye kikundi chao. Vilevile, wataje jambo au mambo makubwa mengine (1-2) ambayo walijifunza kutoka kwenye mada za makundi mengine.

**Nyenzo kwa ajili ya walimu:**

- Utafiti wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa: http://vote.myworld2015.org/

**Darasa la 5 Somo la 3**

"Dini ulimwenguni kote"

**Muda**: Dakika: 60

**Mada:** Urai, Historia, Maarifa ya Jamii

**Viwango:** Elimu Bora ( SDG 4 ); Kupunguza kutokuwepo kwa usawa (SDG 10); Amani, Haki, na Taasisi thabiti ( SDG 16 )

**Imebuniwa na**: Isabelle Byusa, Arianna Pattek, Emily Papa, Sam ( Shiv ) Sharma, Tisha Verma, Devon Wilson

**Muhtasari na Mantiki:** Kuwaweka wazi wanafunzi kwa viongozi wa dini ambao wanatoa michango chanya kwa jamii zao, na kuwezesha majadiliano kwa kuwafanya watafakari na kujibu maswali kwa hekima, busara na heshima wakati wa kujifunza kufanana na kutofautiana kati ya dini za ulimwengu.

**Lengo la Ufundishaji**: Wanafunzi watajifunza juu ya kiongozi maarufu wa dini na kujadili kile alichokifanya kukuza uelewa na uvumilivu wa dini.

**Lengo la Uelewa**:

- Kuchochea uvumilivu kwa dini zote
- Kupata uelewa wa kina na kujitambua

**Maswali Muhimu:**

- Ustahimilivu wa kidini ni nini?
- Dini yako ni ipi (kama unayo) na dini yako inathamini nini?
- Ni viongozi gani wanawakilisha dini za ulimwengu?
- Tunawezaje kujenga uvumilivu na kuheshimu tofauti za kidini?

**Lengo la Ufundishaji** (Wanafunzi wataweza):

- kuzifahamu dini za ulimwengu kupitia viongozi wa dini
- kutafakari juu ya mfanano na utofauti wa dini
- kukuza uwezo wa kuthamini watu wote bila kujali tofauti za kidini

**Tathmini:** "Jedwali la tathmini na udadisi" lenye maswali ya wanafunzi kuhusu dini walizopata fursa ya kuzichunguza..

**Mpangilio wa mazoezi:**

**Anza (Dakika: 20)** kwa kukagua orodha ya dini za ulimwengu. Halafu, endelea kutoa mfano wa dini kubwa na ndogo, ukifuatia na kutoa muhtasari wa:

- msingi wa imani ya dini husika
- Maandiko matakatifu ya dini hizo
- Matamasha na sherehe za dini hizo
- Mavazi rasmi ya dini hizo

**Kisha (kwa dakika 25)** wanafunzi wasikilize rekodi, waangalie video, au wasome maandishi ya kiongozi wa dini ambayo yametoa michango chanya kwa jamii. Mfano ni pamoja na Mahatma Gandhi, Martin Luther King Jr., Mama Teresa, Malala Yousafzai, Aga Khan, nk. Kiongozi wa dini kutoka eneo lao katika jamii ya wanafunzi anaweza pia kuwa mfano wa kutumika kwenye zoezi. Waelekeze wanafunzi wageuke na kuongea na wenzao wakishirikishana walichojifunza kutoka kwa viongozi hawa, na kuwalinganisha na kuwatofautisha na viongozi wenzao wa dini.

**Maswali Muhimu:**

- Je, dini ina mchango gani katika mabadiliko ya jamii?
- Je, dini inaathiri uongozi kwa namna gani?
- Kuna utofauti gani na mfanano gani kati ya viongozi hawa?

**Mwisho (katika dakika 15 za mwisho za darasa**) waelekeze wanafunzi watafakari juu ya somo walilojifunza kwa kumwandikia kiongozi wa dini.

- Miongozo pekee kwa wanafunzi ni kwamba lazima waandike kwa udadisi na heshima, wape changamoto wanafunzi kuandika maswali yao kwa njia ya kuheshimu na kuthamini imani ya kiongozi huyo.
- Baada ya zoezi la kutafakari, wanafunzi watamshirikisha mwalimu maswali yao naye atathibitisha wanafunzi hao ambao maswali yao ni ya kukumbuka, na pia kuwasaidia wanafunzi ambao maswali yao hayana heshima na lugha ya kupendeza kwa kupendekeza maneno ambayo yatafanya maswali yao kuwa yaliyofikiriwa kwa kina, yasiyoegemea upande wowote na ya kidadisi.

**Nyenzo kwa ajili ya walimu:**

- https://www.learningforjustice.org/magazine/teaching-about-religion

**Darasa la 5 Somo la 4**

" Kuchunguza Dini "

**Muda:** Dakika: 60

**Mada:** Uraia, Historia, Marifa ya Jamii

**Viwango**: Elimu Bora (SDG 4); Kupunguza kutokuwepo kwa usawa (SDG 10); Amani, Haki, na Taasisi thabiti (SDG 16)

**Imebuniwa na**: Isabelle Byusa, Arianna Pattek, Emily Papa, Sam ( Shiv ) Sharma, Tisha Verma, Devon Wilson

**Muhtasari na Mantiki:**

- Kipindi kitaanza na zoezi dogo la utafiti wa kikundi ambapo wanaweza kuchunguza mada ya kidini wanayotamani.
- Wanafunzi watawashirikisha wanafunzi wengine utafiti na ugunduzi wao.
- Wanafunzi wanapaswa kushauriwa kuchagua mada ambayo hawaijui kabisa — mada hiyo isihusiane sana na dini yao wenyewe (kama wanafuata dini mojawapo).

**Lengo la Ufundishaji:** Wanafunzi watatafiti mada mpya kuhusu dini na kuwashirikisha wanafunzi wengine matokeo yao.

**Lengo la Uelewa:** Kukuza uvumilivu kwa dini zote na kuelewa misingi ya dini hizo.

**Maswali Muhimu:**

- Una hamu ya kujua nini?
- Tunawezaje kuchunguza na kushirikisha kile tunachojifunza?

**Lengo la Uelewa la Wanafunzi** (Wanafunzi wataweza):

- Kukuza uelewa wa kina na ufahamu wa dini.
- Kukuza ujuzi wa utafiti, uandishi, na ustadi wa uhariri.

**Tathmini**: Kazi ya mwisho baada ya wanafunzi kupokea marekebisho; maoni kutoka kwa mhariri wa jarida la "mwalimu au mwanafunzi darasani."

**Mpangilio wa mazoezi:**

- **Sehemu ya 1**
    - Wanafunzi waulizwe kwanza, "Magazeti yanatengenezwaje? " Hii itasababisha majadiliano juu ya waandishi wa habari na mbinu zao za utafiti kupata habari.

- Kuanzia hapa, mwalimu atawauliza wanafunzi ni nini cha muhimu kuzingatia kama uandishi wa habari (usahihi, kuandika kwa njia ambayo inawavutia watu, athari kwa umma, nk)
- Hapa itaelezwa kuwa darasa linapanga kuanzisha gazeti la shule. Ili kufanikisha hilo, kuna nafasi mbalimbali ambazo zinahitaji kujazwa ( mbunifu wa magazeti, wahariri wa gazeti, nk.) na wanafunzi watahamasishwa kubeba majukumu haya na pia kutumika kama waandishi.

- **Sehemu ya 2**
  - Wanafunzi wataulizwa ni dini gani ambazo zinaweza kupendeza kuripoti; hizi zitaandikwa kwenye ubao. Wanafunzi wataulizwa wana hamu ya kujua nini ndani ya dini hizi, na vikundi vidogo vitaundwa ( k.m. historia, maeneo ulimwenguni kote, nafasi tofauti za uongozi, uhusiano na jamii ya mtu, maadili, sikukuu, nk )
  - Wanafunzi watahamasishwa kuja kwenye ubao na kuandika majina yao kwenye vikundi vyenye mada wanazopendezwa nazo, au kuandika mada mpya ambazo wangependa kuzitafiti katika ulimwengu wa dini.

- **Sehemu ya 3**
  - Wanafunzi watahamasishwa kutengeneza mpango wa utafiti peke yao kwenye kundi la watu wawil, pamoja na:
    - maswali machache / vidokezo vya vitu vinavyowavutia juu ya mada hiyo
    - kutafakari na kuandika juu ya kile ambacho wanafunzi wanakijua tayari kuhusu mada hiyo.
  - Wanafunzi watapewa kipindi chote ili kuanza utafiti wao kwa ajili ya nakala yao ya rasimu ya kwanza inayotakiwa kuwasilishwa ndani ya wiki moja.

- **Sehemu ya 4**
  - Mara tu rasimu itakapokamilika, wanafunzi watapewa maoni ya “mhariri” na wenzao:
    - Je, habari ilikuwa ya kuelemea upande mmoja?
    - Je, ilivuta umakini wa msomaji?
    - Je, haikuwa na makosa ya kisarufi?
    - nk.
  - Halafu wanafunzi watapewa nafasi ya kufanya marekebisho kabla ya habari yao kwenda kwa mhariri wa mwisho (mwalimu).

- **Sehemu ya 5**
    - Kuanzia hapa, mwalimu anaweza kuweka nakala hizo pamoja na kuwashirikisha wanafunzi, au zoezi la ziada linaweza kuundwa ambapo wanafunzi wanaweza kutoa jina la gazeti, na kufikiria na kufanya majaribio ya miundo mbalimbali ya kuhariri habari inayopatikana (mtandaoni kupitia blogu au kupitia machapisho).

- **Sehemu ya 6**
    - Mara mradi utakapokamilika, wanafunzi wataelekezwa kurudi kwenye maelezo yao ya awali na kujibu swali lifuatalo la kutafakari: " Nilikuwa nikifikiria _______________. " " Sasa najua _______________. " (Tazama kiungo cha Mfumo wa Kufikiria unaoonekana hapa chini kwa maelezo zaidi juu ya zoezi hili.)

**Nyenzo kwa ajili ya walimu:**

- Mfumo wa Kufikiria Unaoonekana — Project Zero: https://pz.harvard.edu/projects/visible-thinking

**Darasa la 5 Somo la 5**

"Mawasiliano, Migogoro, na Ushirikiano wa Dini zote"

**Muda**: Dakika: 60

**Mada**: Uraia, Historia, Maarifa ya Jamii

**Viwango**: Elimu ya Bora (SDG 4); Kupunguza kutokuwepo kwa usawa (SDG 10); Amani, Haki, na Taasisi thabiti (SDG 16)

**Imebunia na**: Isabelle Byusa, Arianna Pattek, Emily Papa, Sam ( Shiv ) Sharma, Tisha Verma, Devon Wilson

**Muhtasari na Mantiki:**

Kutumia maarifa kutoka katika masomo ya zamani na kuyatumia kwa hali halisi ya maisha.

**Lengo la ufundishaji:**

Wanafunzi watajadili kukosekana kwa uvumilivu wa kidini katika muktadha wa kufikirika, na kuzingatia jinsi hili linavyoweza kutokea katika maisha yao.

**Malengo ya Uelewa:**

- Jinsi ya kufanya kazi katika mazingira yenye tofauti za kidini
- Jinsi ya kutambua tatizo
- Jinsi ya kufikia makubaliano juu ya suluhisho la amani ambalo linajumuisha maoni ya pande zote zinazohusika (wadau).

**Maswali Muhimu:**

- Mzozo ni nini?
- Je, tunasuluhishaje migogoro kwa amani?

**Malengo ya Kujifunza kwa Wanafunzi (Wanafunzi wataweza):**

- kutoa suluhisho jumuishi
    - Hili linaweza kupimwa kwa ushiriki wa wanafunzi katika darasa na uwasilishaji wa kazi mbele ya darasa
- kufanya kazi kwa tija katika vikundi
    - Hili linaweza kupimwa kwa mwalimu kutazama kazi ya kikundi na tafakari za wanafunzi wakiwa katika mchakato wa kazi za vikundi

**Tathmini**: Muongozo kwa ajili ya uwasilishaji wa kikundi unaotolewa kutoka viwango vya msingi vya darasa la 5 au viwango vya jumla vya kuongea na kusikiliza.

**Mpangilio wa mazoezi:**

**Kabla ya darasa (Dakika: 10)**: Uliza darasa maswali yafuatayo kufungua majadiliano ya darasa; anza kwa vikundi vidogo na kisha ufungue darasa kwa wote:

- Je, mzozo unamaanisha nini?
- Ukosefu wa uvumilivu unamaanisha nini kwako?
- Ni wakati gani umeshuhudia mzozo? Nini kilitokea?
- Je, ni hisia gani ambazo uliziona katika kila upande wa mzozo?
- Walipataje suluhisho?

**Zoezi kuu ( Dakika: 30):** Gawanya wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wasiozidi 4-5. Soma kisa kilichotolewa mbele ya darasa zima, kisha waelekeze wanafunzi wabuni igizo linalosadifu suluhisho bora kuhusiana na kisa walichosomewa.

*Katika nchi ya Zorg, kuna dini kuu 4 za kitaifa. Watu wengi ni wa dini ya Tor. Dini zingine tatu ni Zaria, Mooka, na Bic. Tor na Zaria kimsingi wanapinga wazo la wasichana kwenda shuleni kwa kuzingatia mafundisho yao ya kidini. Mooka na Bic wote wanaamini wasichana wana haki ya kuhudhuria shule waliyopewa na mungu wao. Kwa kuongezea, Zaria, Mooka, na Bic hawahisi kuwakilishwa serikalini, kwani inaongozwa na watu kutoka dini ya Tor. Serikali inajaribu kupitisha sheria kuzuia wasichana kuhudhuria shule kwa sababu ya dini yao. Mooka, Bic, na Zaria wanaamua kufanya maandamano ya vurugu katika mji mkuu wa Zorg ili sauti zao zisikike. Hii inafanya wafuasi wa dini ya Tor kukataa kujadiliana na dini zingine. Je, katika hali hii Utafanya nini?*

**Uwasilishaji na Hitimisho (Dakika: 20):** Wanafunzi wawasilishe masuluhisho yao katika igizo fupi la dakika 3-4 kila mmoja. Mwalimu awaongoze wanafunzi kufanya majadiliano juu ya tafakari binafsi ya mchakato. Ni nini kilienda vizuri? Ulijifunza nini?

**Nyenzo kwa ajili ya wanafunzi:**

- Kutatua hali za migogoro: https://hr.berkeley.edu/hr-network/central-guide-managing-hr/managing-hr/interaction/conflict/resolving